ESRF organizes country-wide forums for post-MDGs future

By Queenter Mawinda

AHEAD of the 2015 deadline to achieve the Millennium Development Goals (MDGs), the Economic and Social Research Foundation (ESRF) has organized an inclusive and participatory cross-section forum to ensure that all stakeholders at different levels are fully involved in providing critical inputs to the Tanzania development agenda and build a shared global vision on the future we want.

Briefing the media in Dar es Salaam yesterday, the ESRF Senior Research Associate Dr Oswald Mashindano, said the forum will be held on Tuesday December 4 at seven sub national (zonal) events to stimulate debate on the future global development agenda and to produce a concrete report on the desired post 2015 development goals that Tanzania has to feed into it.

"The consultation process needs to address new and emerging issues and should be an inclusive, balanced, bottom up and broad based dialogue," he stated.

According to Dr Mashindano, a broad spectrum of stakeholder meetings shall involve representatives from the public sector, government, civil society (to the grassroots level), the private sector, youth and women's groups, people with disability, children and development partners.

The convention will capture the voice and ideas of different sections of the population so as to facilitate a visioning process based on people's experiences of and ideas for the future of the world they want to live in.

Dr Mashindano cited that the MDGs have improved the lives of millions, but there is still much to be done to address extreme poverty, diseases and environmental crises.

"The MDGs have helped to define a common framework of priorities and Tanzania has profoundly changed since MDGs were conceived in 1999 but in some areas like basic needs poverty and child mortality are yet to be overcome," he said.

The eight Millennium Development Goals (MDGs) – which range from halving extreme poverty to halting the spread of HIV/AIDS and providing universal primary education, all by the target date of 2015 – form a blueprint agreed to by all countries and leading development institutions. They have galvanized unprecedented efforts to meet the needs of the world poorest, the researcher noted.

As 2015 approaches questions are growing louder about how far we've come, and what we do next. Discussions on the Post-2015 agenda have begun in light of and as a follow up to the UN Secretary General's report to the 2010 MDGs Summit.

The "post-2015" agenda has already attracted conferences across the world and an avalanche of reports indicating that donors and development experts are already starting to haggle over the future of aid and development.

Some global leaders want to look beyond aid, to unlock wealth through economic growth, trade, tackling corruption, effective government and open societies. It is also argued that it is high time to look for new resources beyond aid to fight poverty.

As part of efforts to define the Post-2015 Development Agenda, the United Nations Development Group (UNDG) has developed a proposal to facilitate a post-2015 consultation process in at least 50 countries (Tanzania being among them) in order to stimulate discussion among respective national stakeholders and to solicit input and ideas that will define a vision of the future world "we want" to live in.

This process is co-led by the United Nations Tanzania Country Office and the government through the Ministry of Finance and the President's Office, Planning Commission.

Newspaper; Guardian

Date; December 1, 2012

As 2015 looms, fears of missing MDGs intensify

By Bernard Lugongo
The Citizen Reporter

Dar es Salaam. As the 2015 deadline for the accomplishment of the Millennium Development Goals (MDG's) approaches, there are fears that the country would miss the target of reducing basic-needs poverty.

Economic and Social Research Foundation (ESRF) noted yesterday that poverty based on lack of basic needs was still a challenge in implementing MDGs in the country.

Senior research associate of the ESRF Osward Mashindano said the basic needs type of poverty has been experiencing a gradual decrease since the country started implementing the MDG as part of the goals ratified by 189 countries.

In the year 1990, this poverty was reduced to 39 per cent, in the year 2000 it decreased to 36 per cent, and to 34 per cent in 2008. The MDGs targets require countries to reduce such poverty to 19.5 by 2015.

"However, Tanzania is one of the countries that has performed well in implementing the goals so far," he said.

On the other hand, Dr Mashindano said the ESRF would in the next one week convene meetings in all seven zones of the country to discuss with stakeholders what the country should do in the post MDG's deadline.

The ESRF was tasked with the duty by the government since the countries that ratified the MDGs were required to have internal discussions on the matter.

Newspaper; Citizen
Date: December 1, 2012

Tz yaelekea kushindwa kutimiza MDG's

Na Debora Sanja, Dodoma

TANZANIA inaelekea kushindwa kufikia Maendeleo ya Malengo ya Milenia (MDGs) ya kupunguza vifo vya akina mama wakati wa uzazi ifikapo mwaka 2015.

Kauli hiyo ilitolewa mjini hapa jana na Mtaalamu Mshauri wa Taasisi ya Utafiti wa Mambo ya Uchumi na Jamii (ESRF), Dk. Rose Mwaipopo.

Alisema hadi mwaka 2010, Tanzania ilikuwa imeshapunguza vifo vya akina mama hadi kufikia vifo 454 kwa kila akina mama 1,000.

"Katika Malengo ya Milenia, inatakiwa hadi kufikia mwaka 2015 vifo vya akina mama wakati wa uzazi viwe vimepungua hadi vifo 133 kati ya akina mama 1,000 lengo ambalo hadi sasa sio rahisi kulifikia.

"Sababu kubwa ya kutofikia lengo hilo ni kuwapo kwa akina mama ambao bado wanajifungulia kwa wakunga wa jadi badala ya kuhudumiwa hospitalini," alisema Dk. Mwaipopo.

Alisema lengo ni kufikia asilimia 90 ya akina mama wanaopewa huduma za uzazi na wahudumu wa afya ifikapo mwaka 2015.

Alisema hadi mwaka 2010, asilimia 50.5 ya akina mama ndio waliokuwa wakihudumiwa na wahudumu wa afya wakati wa uzazi, hali ambayo haiwezekani kufikia Malengo ya Milenia ifikapo mwaka 2015.

Alitaja malengo mengine ambayo yanaelekea kutofanikiwa kuwa ni pamoja na suala la usalama endelevu wa mazingira, kupunguza na kuondoa ufukara na njaa ikiwamo kushindwa kupunguza idadi ya watoto wa umri wa miaka mitano waliodumaa.

Alisema malengo yanayoelekea kufanikiwa ni pamoja na kufanikisha elimu ya msingi, kuinua haki za kijinsia na kuwawezesha wanawake na kupunguza vifo vya watoto.

"Malengo mengine yanayoelekea kufanikiwa ni kupambana na Virusi Vya Ukimwi, malaria na maradhi mengine na kuendeleza ushirikiano wa kimataifa," alisema Dk. Mwaipopo.

Alisema lengo la mkutano huo ni kusikiliza maoni ya wadau ikiwamo kuibua changamoto katika kufikia malengo hayo na kuzifikisha Ofisi ya Rais Tume ya Mipango kwa ajili ya kuzifanyia kazi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa, Dk Rehema Nchimbi, aliwataka wadau hao wakati wakijadili malengo hayo wasizichukie changamoto zilizopo badala yake wapendekeze nini kifanyike.

"Kitu chochote kizuri kikiwa kinafanyika, lazima kuwapo na changamoto hivyo tuangalie nini kifanyike ili kukabiliana na changamoto hizo," alisema Dk. Nchimbi.

HABARILEO JUMATANO DESEMBA 5, 2012

Malengo ya Millenia kufikiwa kwa Watanzania kujiajiri-RC

Na Grace Chilongola, Mwanza

WATANZANIA wametakiwa kufanya kazi za kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa, ili kuisaidia Tanzania kufikia Malengo ya Millenia ya mwaka 2015.

Mwito huo ulitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Evarist Ndikilo wakati alipokuwa akifungua mjadala wa wadau wa mchakato wa maendeleo baada ya Malengo ya Millenia 2015 mjadala unaosimamiwa na Taasisi ya Utafiti wa Mambo ya Jamii na Uchumi (ESRF).

Alisema kuwa tangu kuanzishwa kwa mpango wa Millenia, hadi sasa yapo baadhi ya malengo

Evarist Ndikilo

yamefikiwa huku baadhi ya maeneo yakiwa na changamoto ambazo bila kuwa na ushirikiano kati ya Serikali na jamii, hayatofikiwa.

Ndikilo alisema kuwa uchumi wa nchi unategemea kilimo kutokana na kuwa na ardhi kubwa yenye rutuba katika kilimo na kuwasisitizia wananchi kulima kilimo cha kisasa.

"Tuna ekari 32,615 za ardhi kwa ajili ya kilimo lakini kiasi kinachotumika ni ekari 1,008 tu ambacho ni kidogo ukilinganisha na ambacho kimebaki bila kutumiwa," alisema Ndikilo.

Kwa upande wa uchimbaji wa madini, alisema kuwa umefika wakati kwa wachimbaji kuiingizia Serikali mapato kwa kulipa kodi na ndiyo maana Serikali imejipanga kuwasaidia ili wafanye kazi hiyo kwa njia za kisasa ambapo imetenga Sh bilioni 8.9 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa.

Alisema kutokana na umuhimu wa sekta hiyo katika kuhakikisha Malengo ya Millenia yanafikiwa, Serikali imekuwa ikiweka mkono wake ili kuyafanikisha.

Mkuu wa Utafiti kutoka ESRF, Donatila Kaino alisema kama nchi itakuwa na umeme wa uhakika, uchumi wa nchi utakua kutokana na wakulima kutumia fursa hiyo kuongeza thamani ya mazao yao.

Aidha alisema changamoto ya masoko ifanyiwe kazi ili mkulima awe na uhakika wa soko la mazao yake mara baada ya kuvuna pamoja na uhakika wa miundombinu ya kusafirishia.

Kilimo kinahitaji bajeti kubwa, yasema ESRF

Na John Nditi, Morogoro

SERIKALI imeshauriwa kutenga bajeti kubwa na kuweka nyenzo muhimu kwenye sekta ya kilimo ambayo ni mhimili mkuu wa kuajiri watu wengi na kuchangia pato la Taifa.

Mshauri Mwelekezi wa Taasisi ya Utafiti katika Uchumi na Jamii (ESRF), Deo Mutalemwa, alisema hayo jana mjini hapa kabla ya kumkaribisha Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Joel Bendera kufungua warsha kuhusu maoni ya namna ya kutimiza Malengo ya Millenia.

Akizungumza na wadau hao wa Serikali za Mitaa na asazi za kiraia wa Kanda ya Mashariki kwa mikoa ya Pwani, Iringa na Morogoro, Mutalemwa alisema mkazo huo katika kilimo pia utapunguza umasikini kwa asilimia 80 ya wananchi wanaotegemea kilimo kama njia kuu ya kuinua kipato. "Kilimo ni mhimili mkuu kwa asilimia 75 na ukuaji wake kwa mwaka ni kati ya asilimia 3-4, huko ndiko watu wengi wapo, wanategemea sekta hii katika uzalishaji utakaowapatia ajira na ndiyo yenye uwezo wa kuwakwamua wananchi kuondokana na umasikini," alisema Mshauri Mwelekezi huyo.

Alisema umasikini umepungua kidogo ikilinganishwa na ukuaji wa uchumi wa taifa unaofikia kwa mwaka asilimia 6.7 hadi 7.1.

Hata hivyo alisema kumekuwepo na mafanikio makubwa ya kupunguza umasikini kwa Watanzania kwa mujibu wa takwimu za Malengo ya Millenia nchini Tanzania kutoka asilimia 39 mwaka 1990, hadi asilimia 34 mwaka 2008. Hata hivyo alisema lengo ni kupungua hadi kufikia asilimia 19.2 mwaka 2012.

Alitaja baadhi ya changamoto zinazochangia kujitokeza kwa umasikini kuwa ni pamoja na mgawanyo wa rasilimali za anchi kutolingana na kipato cha watu, matumizi mabaya ya fedha na ukusanyaji usioridhisha wa mapato. Alifafanua kuwa ukusanyaji huo wa mapato umekuwa ukiwalenga wafanyabiashara wadogo na kuwaacha wakubwa wenye viwanda ambao wamekuwa wakinufaika na misamaha mingi ya kodi. Kwa mujibu wa Mshauri Mwelekezi huyo, ufisadi mpana pia umechangia kushindwa kupunguza umasikini kwa wananchi.

Naye Bendera, alisema Tanzania imeelekeza sera na mipango yake ili kufikia malengo yaliyowekwa pamoja na mafanikio makubwa yaliyofikiwa ikiwemo kuondoa ada ya elimu ya msingi ambayo imeongeza idadi ya watoto wanaoandikishwa kuanza shule za msingi.

UCHUMI & BIASHARA U&B

Kasi ya kupungua umaskini nchini yawa ya kusuasua

Na Aziz Msuya, Morogoro

UMASKINI nchini umetajwa kupungua kwa kasi ndogo ikilinganishwa na puto la taifa kutokana na sekta ambazo zinategemewa kwa kiasi kikubwa kukuza uchumi wa nchi kuwa haziajiri watu wengi.

Hayo yalisemwa na Mshauri Mwelekezi wa Taasisi ya Utafiti wa Uchumi na Jamii (ESRF), Deo Mutalemwa, katika warsha ya kukusanya maoni ya wadau wa Serikali za Mitaa na Asasi za Kiraia kuhusu Malengo ya Milenia iliyofanyika mwanzoni mwa wiki hii mjini Morogoro ambapo alizitaja sekta hizo kuwa ni madini, utalii, viwanda na ujenzi.

Alisema sekta hizo haziajiri watu wengi kwa sababu ya maendeleo ya matumizi ya teknolojia ambayo inawafanya wafanyakazi kupungua na kwamba pamoja na uchumi kukua kutoka asilimia 6.7 hadi 7.1 kuanzia mwaka 2,000 hadi 2012, lakini umaskini haujapungua kama ambavyo ilitarajiwa katika malengo ya milenia.

"Kuanzia mwaka 2000 hadi 2008 umaskini umepungua kwa asilimia 5 tu kutoka asilimia 39 hadi 34 kiwango ambacho ni kidogo sana kwenye kupambana na umaskini," alisema Mutalemwa.

Mutalemwa alisema kilimo ambacho kinaajiri Watanzania kwa asilimia 75 kinakua kwa asilimia tatu hadi nne ukuaji ambao ni mdogo kulinganisha na sekta zingine ambazo zinakuza uchumi na akasisitiza kwamba ili kukuza uchumi ni lazima Serikali iongeze wigo wa ukusanyaji wa kodi, kuziba mianya ya uvujaji wa fedha na kupunguza misamaha ya kodi.

Alisema sekta binafsi ni lazima ilipe kodi kikamilifu kuliko ilivyo hivi sasa, ambapo kodi inalipwa na kundi dogo la wananchi ambao wanalipa kodi kidogo na akashauri kwamba njia nzuri ya kukabiliana na ufisadi ni kuwa na mifumo imara ya matumizi ya fedha za umma ikiwa ni pamoja na kuzingatia maadili ya utumishi wa umma kuanzia ngazi ya chini kabisa.

Malengo ya maendeleo ya milenia 2000-2015 yalikuwa na lengo la kuhakikisha rasilimali za nchi zinatumika kuboresha maisha ya Watanzania na utekelezaji wake unafanyika kupitia sera na mikakati ya Kitaifa ambapo hadi kufikia mwaka 2008 uandikishaji wa watoto katika Shule za Msingi umefikia asilimia 97 mwaka 2008 kutoka asilimia 54 mwaka 1990, wakati lengo ni kufikia asilimia 100 mwaka 2015.

Vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka watoto 115 kati ya watoto 1,000 mwaka 1990 hadi watoto 68 kati ya watoto 1,000 mwaka 2008 lengo likiwa ni kupunguza vifo hivyo hadi watoto 38 kati ya watoto 1,000 mwaka 2015, wakati umaskini wa huduma muhimu umepungua kutoka asilimia 39 mwaka 1990 hadi asilimia 34 mwaka 2008 lengo likiwa ni kufikia asilimia 19.5 mwaka 2015.

Mapema akifungua warsha hiyo Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Joel Bendera alisema Malengo ya Milenia ni matokeo ya Mkutano wa Umoja wa Mataifa uliofanyika Septemba 9 mwaka 2000 na kuwakutanisha wakuu wa chi 147 ambao waliwakilisha mataifa wanachama 189 wa Umoja wa Mataifa lengo likiwa ni kufafanua mkakati wa pamoja wa vipaumbele juu ya jinsi ya kukidhi mahitaji ya umaskini duniani.

Newspaper; Mwananchi

Date; December 6, 2012

'Changamoto ni nyingi kufikia malengo 2015'

Sheilla Sezzy, Mwanza

WAKATI ikiwa imebakia miaka mitatu ili kukamilisha utekelezaji wa malengo ya milenia ya mwaka 2015 ,Tanzania bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ili kufikia malengo hayo ikiwemo ukuaji wa uchumi wa nchi.

Hayo yamebainishwa jana na Mkuu wa Utafiti kutoka ESRF, Donatila Kaino alipotoa mada kwa wadau wa maendelea na kusema kuwa, pamoja na Serikali kutoa fursa za maendeleo lakini hali bado siyo nzuri kwa ukuaji uchumi wa nchi pamoja na kipato cha mtu mmoja mmoja.

Alitoa ufafanuzi kwa kusema kuwa, umaskini wa huduma muhimu umepungua kutoka katika asilimia 39 katika kipindi cha mwaka 1990 hadi asilimia 36 katika mwaka 2000/08 ambapo ilifikia asilimia 34.

Aliendelea kwa kusema kuwa, malengo ya milenia yanasisitiza zaidi maeneo ya afya, elimu , mazingira na ustawi wa jamii kwa jumla.

Alisema kwa mtazamo huo bado kuna changamoto nyingi katika kuhakikisha maeneo hayo yanaenda sawa na malengo hayo.

Kwa upande wa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Evarist Ndikilo amewataka Watanzania kujenga tabia ya kufanya kazi baada ya kusubiri kuajiriwa ili kuweza kuisaidia Tanzania kufikia malengo ya millenia ya mwaka 2015.

Newspaper; Majira

Date; December 6, 2012

Malengo ya milenia hayaendani na mipango

Na Patrick Mabubula, Shinyanga

UTAFITI kuhusu kupata maoni baada ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia kufikia mwaka 2015 umebainisha kuwa malengo hayo hayaendani na mipango mikakati katika kupunguza umasikini kwa jamii.

Hayo yameelezwa juzi na mtafiti wa mambo ya uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Der es Salaam, Dkt. Oswald Mashindano katika lengo la kukusanya maoni kwa wananchi, viongozi wa Serikali, asasi zisizokuwa za kiserikali katika warsha ya siku moja iliyofanyika mkoani Shinyanga.

Dkt. Mashindano aliwataka wadau wa maendeleo kueleza katika tafiti nini kifanyike baada ya malengo ya milenia ya 2015 yaliyosababisha kutofanikiwa vema.

Katika warsha ya majadiliano na wadau kuhusu ajenda ya maendeleo yaliyojumuisha mikoa minne ya Kanda ya Magharibi ukiwemo Kigoma, Simiyu, Shinyanga na Tabora walisema rushwa, ufisadi, uwajibikaji ubovu katika kutekeleza sera zinazotungwa ni sehemu ya sababu zinazofanya kutofikiwa vizuri kwa malengo hayo mwaka 2015.

Aidha, Charles Maugira ambaye ni Ofisa Tarafa Shinyanga Mjini alisema, kutofikiwa vizuri kwa malengo ya maendeleo ya milenia kufika mwaka 2015 ni Watanzania kutokuwa makini katika shughuli mbalimbali hasa kujibidiisha katika uchumi.

Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu Mkoa wa Kigoma, Georges Bussungu alisema baada ya malengo ya milenia ya 2005 ilipaswa iwekwe sheria ngumu kuhusu miiko ya uongozi itakayodhibiti wale wanaoonekana wabovu na wasiokuwa wawajibikaji.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Annarose Nyamubi wakati wa kufungua warsha hiyo alisema kila mmoja achukue nafasi yake kuanzia Serikali, viongozi wa madhehebu ya dini, asasi za kiraia na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kufanikisha malengo ya hayo mwaka huo.

Wakati huo huo, Dkt. Mapambano alisema vigezo vya kukua kwenye uchumi wetu hapa nchini vimekuwa vikitumika katika uwekezaji wa viwanda, madini, utalii badala ya kuupima kwenye sekta ya kilimo ambako ndiyo jamii inaishi kwa kwa asilimia 100 ya maisha yao.

Print

6th December 12

THISDAY
:: The voice of transparency ::

Mtaalam aeleza kwanini Tanzania ni maskini

Ashton Balaigwa

Imeelezwa kuwa kasi ndogo ya kupungua kwa umasikini nchini inatokana na sekta zinazoendesha uchumi kutoajiri watu wengi.

Hayo yamesemwa na Mshauri Mwelekezi wa Taasisi ya Utafiti wa Masuala ya Kiuchumi na Kijamii (ESRF), Deo Mtalemwa, wakati akizungumza katika warsha ya siku moja ya kutoa maoni ya wadau wa serikali za mitaa na asasi za kiraia juu ya malengo ya milenia (MDG), mjini hapa jana.

Mtalemwa ambaye amefanyakazi na Benki ya Afrika (ADB) kama Afisa Mikopo na Afisa Uhusiano kwa miaka 20, alisema sekta za msingi zinazoendesha uchumi wa nchi kama vile, madini, viwanda, ujenzi na utalii zimeajiri idadi ndogo ya Watanzania ikilinganishwa na sekta ya kilimo ambayo licha ya kuajiri idadi kubwa ya watu lakini imekosa msukumo wa kutosha kuchangia ukuaji wa uchumi.

Sababu nyingine alizotaja kukwamisha jitihada za Tanzania kupunguza umasikini ni, kuwepo kwa migawanyo mibovu ya rasilimali za nchi, baadhi ya mikoa kuwa na rasilimali nyingi na mingine ikiwa haina rasilimali za kutosha na kuwepo kwa mifumo mibovu ya ukusanyaji kodi na usimamizi wake.

Alisema ili kukabiliana na changamoto hizo, ni lazima Tanzania ikapanua wigo wa ukusanyaji kodi ili Watanzania wote walipe kodi na kutolea mfano wa posho za vikao mbalimbali kuwa zimekuwa zikitolewa pasipo kukatwa kodi jambo ambalo alidai ni eneo jingine linaloweza kupanua wigo wa kodi.

Aidha, Mutalemwa aliwataka Watanzania kutotumia njia za ujanja ujanja kukwepa kodi badala yake walipe kodi kwa hiari ili kujenga ujasiri wa serikali wa kuhoji pale ambapo wanaona matumizi ya fedha zao hayafanywi kwa usahihi.

Hata hivyo, alisema Tanzania imefanya vizuri katika kukuza uchumi wake kutoka asilimia 6.8 mwaka jana hadi kufikia asilimia 7.1 mwaka huu.

Alisema utafiti uliofanywa na Umoja wa Mataifa umebaini kuwa, umasikini nchini umepungua kwa asilimia 5 katika kipindi cha miaka 18 toka mpango wa milenia wa kupunguza umasikini duniani ulipopitishwa na mataifa 189 Tanzania ikiwemo na kuanza kufanyiwa kazi mwaka 1994 mpaka sasa.

Takwimu za umoja huo zinaonyesha uchumi wa Tanzania umekuwa kwa asilimia 7.1 mwaka huu toka asilimia 6.8 mwaka 2011, huku Uganda ikionyesha uchumi wake kukua kwa kasi zaidi kwa toka asilimia 4.1 mpaka kufikia asilimia 6.0.

Nchi nyingine katika ukanda wa Afrika Mashariki ni Rwanda ambayo uchumi wake umekua kwa asilimia 9.9 kutoka asilimia mwaka 2011 hadi asilimia 8.8 mwaka huu, huku Burundi ukikua kwa 4.8 mwaka huu toka asilimia 4.2 mwaka jana.

Kwa upande wa Kenya, uchumi wake unaonyesha kushuka kwa asilimia 1.6 kutoka asilimia 5.1 mwaka jana hadi asilimia 3.5 mwaka huu.

NIPASHE

'Umaskini bado ni tatizo nchini'

Shija Felician, Shinyanga

SERIKALI imekiri kuwa umaskini bado ni mzigo mkubwa kwa Watanzania licha ya kuwepo kwa mipango mingi ya kuuondoa tatizo hilo.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Ally Rufunga, wakati akifungua warsha ya mchakato wa kukusanya maoni kuhusu malengo ya maendeleo baada ya milenia, iliyoshirikisha Mikoa ya Tabora, Kigoma, Shinyanga na Simiyu.

Katika hotuba yake iliyosomwa na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Annarose Nyamubi, mkuu huyo wa mkoa alisema na mikakati hiyo bado maisha ya wananchi ni duni.

Mkuu huyo wa mkoa alisema wananchi wa vijijini hata wakiulizwa maana ya Mkukuta hawajui na kwamba hiyo ni kwa sababu hakuna mkakati wa pamoja wa kuhakikisha kuwa mpango huo unawafikia.

Aliwataka wanahabari kufikisha ujumbe sahihi kwa wananchi ili baada ya mwaka 2015, Watanzania wote wawe na mabadiliko kulingana na malengo ya millennia hasa katika sekta za elimu, afya, miundo binu ya barabara na kadhalika.

Mtafiti wa Uchumi, Dk Oswald Mashindano, alisema udhaifu wa sera ndiyo sababu mojawapo inayoongeza umaskini.

Newspaper; Mwananchi

Date: December 6, 2012

Newspaper; Mwananchi
Date; December 7,2012

Tanzania yakwama kufikia Malengo ya Milenia 2015

Habel Chidawali, Dodoma

JUHUDI za Tanzania kufikia malengo ya Milenia zinaelekea kukwama, ikiwamo kupunguza vifo vya wanawake wakati wa uzazi ifikapo mwaka 2015.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Mtaalamu Mshauri wa Taasisi ya Utafiti wa Mambo ya Uchumi na Jamii (ESRF), Dk Rose Mwaipopo inaonyesha juhudi hizo zikó nyuma licha ya mikakati mingi iliyowekwa na Serikali.

Dk Mwaipopo alikuwa akizungumza kwenye mkutano wa wadau wenye lengo la kuibua changamoto na mafanikio kuelekea kutimiza malengo ya milenia ya mwaka 2015, uliofanyika kikanda mkoani Dodoma.

Mtaalamu huyo alisema hadi mwaka 2010, Tanzania ilikuwa imepunguza vifo vya wanawake hadi kufikia 454 kwa kila wanawake 1,000.

Alisema malengo ya milenia inatakiwa hadi kufikia mwaka 2015 vifo vya wanawake wakati wa uzazi viwe vimepungua hadi 133 kati ya 1,000, lengo ambalo hadi sasa inakuwa ni vigumu kulifikia.

"Sababu kubwa ya kutofikia lengo hilo ni kuwapo kwa wanawake ambao wanajifungulia kwa wakunga wa jadi badala ya kuhudumiwa hospitali," alisema Dk Mwaipopo.

Alibainisha kuwa katika malengo ya milenia, ilikuwa ni kufikia asilimia 90 ya wanawake wanapewa huduma za uzazi na wahudumu wa afya ifikapo mwaka 2015.

Taarifa hiyo inaonyesha hadi mwaka 2010, asilimia 50.5 ya wanawake ndiyo waliokuwa wakihudumiwa na wahudumu wa afya wakati wa uzazi, hali ambayo haiwezekani kufikia malengo ya milenia ifikapo mwaka 2015.

Newspaper; Nipashe
Date: December 7. 2012

ESRF kujadiliana na wadau Malengo ya Milenia

Na Daniel Mkate

TAASISI ya Utafiti wa Uchumi na Jamii (ESRF), katika kuelekea Malengo ya Milenia (MDGs), imejipanga kufanya majadiliano na wadau mbalimbali wakiwemo watu wenye ulemavu na akinamama ili kujua kero zinazozikumba jamii.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mtafiti Mshiriki wa ESRF, Dk. Oswald Mashindano, alisema serikali imeona iwahusishe wadau wa kada za kawaida ili kujua kipi cha kufanya kuelekea malengo ya Milenia.

"Tutaanza katika kanda saba wiki ijayo kufanya majadilio na wadau wa kada mbalimbali hususani wale wasio na fursa kama walemavu, akinamama wa kawaida, wenye kipato cha chini na vijana," alisema Dk. Masumbuko.

Dk. Masumbuko alisema malengo ya majadiliano hayo katika kanda hizo saba watakazotembelea ni kutaka kujua vifo vya akina mama, elimu, fursa sawa, njaa na umaskini unaowakabili watu wa kada hizo.

Alisema baada ya utafiti walio ufanya, wamegundua kuna mambo mengi ambayo jamii ya kawaida inaweza kusaidia kutoa mawazo yao katika utaratibu wa MDGs, hivyo kuamua kufanya majadiliano na wadau hao ili kuweza kugundua matatizo yanayowalenga.

Mtafiti huyo alisema pamoja na majadiliano hayo, pia wataangalia michakato ya kimaendeleo katika jamii inavyokwenda.

Alitaja kanda ambazo watafanya majadiliano hayo na wadau mbalimbali kuanzia Jumanne ijayo ni Kanda ya Ziwa inayojumuisha mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara na Geita, huku Kanda ya Kaskazini ikiwa na mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Tanga.

Kanda nyingine ni Kati ambayo itajumuisha mikoa ya Dodoma, Manyara na Singida, Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Njombe na Katavi wakati Kanda ya Kusini ikihusisha mikoa ya Mtwara na Lindi na Kanda ya Mashariki ikiwa na Morogoro, Iringa na Pwani na ile ya Magharibi ikiwa na Shinyanga, Simiyu, Kigoma na

TANZANIA VIS-A-VIS UNITED NATIONS MDGs: Poverty declines by only five per cent in ten years. Fast-growing sectors employing too few people

Written by AZIZ MSUYA

Saturday, 08 December 2012 10:01

MOROGORO?Poverty in Tanzania has decreased by only five per cent – a relatively small percentage point –in ten years of earnest pursuit of the 15-year Millennium Development Goals (MDGs) programme whose span comes to an end in 2015.

The top priority of the Goals, a United Nations-backed initiative, is the 'reduction of basic needs poverty.'

Despite economic growth rising from 6.7 per cent in the year 2000 to 7.1 per cent in 2012, poverty reduction was marginal in the face of MDGs aspirations.

Researchers at the Economic & Social Research Foundation (ESRF) say that, in terms of the country's gross domestic product (GDP), poverty has not been significantly dented despite much-vaunted economic growth. This, the researchers explain, is basically because the sectors of the economy which are experiencing fast growth on the ground do not employ many people.

Noting that the fast-growing sectors are mining, tourism, industry/manufacturing and construction, an ESRF consultant, Deo Mutalemwa, said that, for example, "manufacturing doesn't employ many people because technological improvements lead to staff reductions!"

Mutalemwa was addressing participants in a special workshop convened in Morogoro municipality this week to gather the views of stakeholders in local government and civil society on the way forward after the current Millennium Development Goals programme ends.

"From the year 2000 to 2008, poverty was reduced by only five per cent, coming down from 39 to 34 per cent," Mutalemwa said, adding that this was too small a scale to fight poverty effectively and sustainably!

Agriculture – an important sector of the economy which engages 75 per cent of the workforce – has been growing by a mere 3-to-4 per cent annually, which is a very small growth rate compared to the other sectors. This is not enough to offset poverty on the ground.

Commenting on the way out and forward, Mutalemwa said that, in order to boost the economy, the government should increase its scope of tax collections, plug the rampant leakage of public funds, and reduce the proliferation of tax exemptions.

Also, the private sector should contribute more fully in the form of taxation than is the case today, whereby the range of fully committed taxpayers is very narrow, surrounded by many potential taxpayers who either pay very little tax or none at all!

Then there is a great need to tackle the rampant grand corruption head-on, and ensure stable patterns of public funds use.

At the turn of this century, the United Nations Organisation urged the developed and developing countries to work together to achieve the noble goals of reducing poverty, hunger, disease, and deaths of expectant mothers and children under five years of age.

Other priorities were free primary education for all children; equal opportunities for women, and creating an environmental framework for sustainable development.

Targets of the Millennium Development Goals (2000-2015) are to ensure that resources are used to improve the lives of the majority of the people. Implementation of this was to be done through definitive policies and strategies.

In Tanzania, these massive enrollment of children in primary schools which saw up to 97 per cent enrollment in 2008, up from 54 per cent in 1999. The objective in terms of the MDGs is to reach 100 per cent enrollment by or in 2015!

Infant mortality has dropped from 115 children dying out of every 1,000 children born alive, to 68 children dying out of 1,000 by 2008. The MDG aim is to halve the remaining deaths of children to 38 out of 1,000 births by 2015.

'Essential services' poverty decreased from 39 per cent in 1990 to 34 percent in 2008, with plans of reaching 19.5 per cent remaining on the cards by 2015.

In his opening remarks at the workshop, the Morogoro regional commissioner, Joel Bendera, said the Millennium Development Goals sought to define a common framework for priorities on how to meet the needs of people touched by global poverty.

JAMBO LEO
Ijumaa Januari 4, 2013

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Rehema Nchimbi.

Dk Nchimbi: Tushirikiane kufikia malengo ya Milenia

■ Na Joyce Kasiki

MALENGO ni jambo la msingi katika maisha iwe kwa mtu mmoja mmoja, vikundi, taasisi au Serikali.

Kwa kuwa na malengo ndipo mtu,shirikaamataasisiinaweza kusonga mbele kwa kuwa atakuwa anafanya kazi huku akiangalia kile alichojipangia kama kinafanikiwa au la.

Kwa maneno mengine naweza kusema malengo ni muongozo wa kufikia katika hatua fulani iliyopangwa kwa ajili ya kujipatia maendeleo zaidi au kupiga hatua moja hadi hatua nyingine.

katika jamii hapa nchini.

Malengo hayo ya Mileniani matokeo ya mkutano wa kilele wa Milenia wa Umoja wa Mataifa uliofanyika Septemba mwaka 2000 na ambao uliwakutanisha pamoja wakuu wa nchi 147 waliokuwa wakiwakilisha mataifa wanachama 189 wa umoja huo.

Lengo kuu la mkutano huo lilikuwa ni kufafanua mkakati wa pamoja wa vipaumbele kuhusu namna ya kuondoa umasikini duniani na kuleta maendeleo katika jamii.

Akizungumza katika warsha ya wadau ya kukusanya maoni kuhusu Malengo ya Mendeleo ya Milenia baada na mazingira bora ya kuunga mkono maendeleo endelevu.

"Tanzania ni kati ya nchi zilizoitikia mwito wa Malengo ya Milenia, na imefanya vizuri katika maeneo mengine, ingawa matokeo katika baadhi ya maeneo si ya kuridhisha. Hizi ni changamoto tu ambazo tunapaswa kukabiliana nazo," anasema Dk.Nchimbi

Akitolea mfano kuhusu changamoto hizo, Dk.Nchimbi anasemaumasikiniwahuduma muhimu umepungua kutoka asilimia 39 mwaka 1990 hadi 33.6 mwaka 2007, wakati lengo lilikuwa ni kupunguza umasikini huo hadi kufikia asilimia 19.5 ifikapo mwaka 2015.

vifo hivyo hadi kufikia vifo 38 katika watoto 1000 ifikapo mwaka 2015.

"Haya ni baadhi ya mafanikio yaliyoonekana hapa nchini, ingawa hata hivyo, umasikini hapa nchini umepungua kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na kukua kwa pato la taifa ambalo limeongezeka kutoka asilimia 1.6 mwaka 1992 hadi kufikia asilimia 7.0 mwaka 2010,

"Na hili ndilo tatizo kubwa linaloonekana kuendelea kuathiri maendeleo na ustawi wa jamii yetu hapa Tanzania," anasema Dk.Nchimbi

Hata hivyo anasema changamoto katika eneo lolote ni muhimu kwani zinatoa mwanga wa nini kifanyike

Katika kuhakikisha Tanzania inapata maendeleo na kuondokana na mambo mbalimbali yaliyoonekana kuwa changamoto na kurudisha nyuma maendeleo yake, iliamua kujiwekea mikakati ya kupambana na changamoto zinazoikabili.

Na hapo ndo ilipojiwekea Malengo ya Milenia katika muda mfupi wa kati na mrefu ili kuona namna ya kukabiliana na mambo ambayo yamekuwa changamoto na kero kubwa ya 2015 Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk.Rehema Nchimbi anasema, mpango wa malengo ya Milenia unataka mwito kwa nchi zinazoendelea na zilizoendelea kufanya kazi kwa kushirikiana ili kufikia malengo ya kupunguza umasikini, njaa, magonjwa pia kupinga za vifo vya akina mama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Lakini pia kuhakikisha elimu ya msingi kwa watoto, fursa sawa kwa wanawake

Kuhusu masuala ya elimu anasema, uandikishwaji wa watoto katika shule za msingi umeongezeka kutoka asilimia 54.2 katika mwaka 1990 hadi kufikia asilimia 95.4 mwaka 2010 huku lengo likiwa ni kufikia asilimia 100 ifikapo mwaka 2015.

Na vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka watoto 115 kwa 1000 mwaka 1990 hadi 51 kwa watoto 1000 katika mwaka wa 2010 huku lengo kuu likiwa ni kupunguza

"Changamoto ni sawa mtu anapojisikia homa katika mwili wake, bii homa au kutojisikia vizuri ndiko kunakomfanya mtu aende hospitali ili kuona nini kinachomsumbua,

"Na akijua kinachomsumbua, tayari anaanza kulikabili tatizo, kwa hiyo hata sisi kupata changamoto ni hatua nzuri ambayo inatuongoza kwamba katika maeneo ambayo hatukufanya vizuri, tufanye

hivyo," anasema.

Anasema utekelezaji wa Malengo ya Milenia umekuwa ukifanyika kupitia utekelezaji wa sera na mikakati ya Kitaifa hukuakitoleamfanoutekelezaji wa Dira ya Taifa 2025 na Dira ya Zanzibar 2020 ni utekelezaji wa Malengo ya Milenia kwa kiasi fulani.

Anasema utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na kuondoa Umasikini Tanzania (Mkukuta) wa kwanza na wa pili, pamoja na Mpango wa Maendeleo wa muda mrefu 2010-2025 pamoja na Mipango ya maendeleo ya muda wa Kati 2010-2015, 2015-2020 na 2020-2025, ni sehemu kubwa ya utekelezaji wa Malengo ya Milenia. •

"Kwa kuwa sasa hivi tunakaribisha kufikia mwaka wa Malengo ya Milenia mwaka 2015, bado takriban miaka mitatu na kwa kuwa baadhi ya nchi bado hazielekei kuyafikia Malengo ya Milenia ifikapo 2015 Kama tunavyotegemea.

"Watu na taasisi mbalimbali duniani wameshaanza kujadili na kujiuliza kitatokea nini baada ya mwaka 2015, wengine wameulizia nini kifanyike baada ya kipindi hicho ili kuongeza kasi ya kutoa msukumo wa maendeleo duniani," anasema

Anasema kutokana na maswali hayo, imesababisha Serikali kuagiza wadau mbalimbali nchini kushirikishwa katika majadiliano hayo ili watoe vipaumbele vya kitaifa na kupanga mikakati endelevu ambayo wadau wenyewe wanaamini itakuwa na ufanisi.

"Taarifa itakayotokana na majadiliano haya, itakuwa mchango wa Tanzania katika kuandaa mikakati mpya na malengo mapya tunayoamini yapata msukumo wa kimaendeleo duniani kote hususan katika nchi husika," anasema.

Anasema katika kutekeleza hilo, Taasisi ya Utafiti wa Mambo ya Uchumi na Jamii (ESRF) imepewa jukumu na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kukusanya maoni ya wadau kupitia warsha hapa nchini.

Anasema warsha hizo zimekutanisha wadau na